# MAJUKUMU YA BODI MBALIMBALI KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Mkutano wa RMO/DMOs –LAPF Dodoma

13 Agosti, 2018

# Mtiririko wa Mada

1. Utangulizi
2. Muundo wa Bodi/Kamati
3. Hali halisi ya Utendaji wa Bodi na Kamati: Mafanikio na Changamoto
4. Usimamizi katika Halmashauri
5. Nini kifanyike kuimarisha Bodi na Kamati

# Utangulizi

- Mabadiliko katika Sekta ya Afya yanayoendelea yana lengo la kuinua kiwango cha ubora wa huduma, kuongeza uwajibikaji kwa wasimamizi na watoa huduma.
- Ili kufanikisha leongo hilo, madaraka, majukumu, kazi na rasilimali za afya zilipelekwa kwa wananchi katika ngazi za utoaji huduma
- Mwaka 1994 iliamliwa ziundwe Bodi (CHSB) na Kamati (HFGC) kama vyombo vya kuwakilisha jamii katika kusimamia huduma za afya.

# Utangulizi,…

- Bodi na Kamati za Huduma za Afya katika Halmashauri ziliundwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Wilaya, Sura Na. 287 na Sheria ya Mamlaka za Miji, Sura Na. 288.
- Sheria hizo zinazipa Halmashauri mamlaka ya kuunda Bodi za Huduma za Afya na Kamati za Vituo vya Huduma

# Utangulizi,…

Hivyo, bodi zinawajibika katika Halmashauri zake na zinatekeleza kazi zake kama ilivyoainishwa katika **Hati Rasmi.**

Hati Rasmi  zinaainisha kipindi cha bodi kuwa madarakani, uhusiano na jamii wadau mbalimbali, majukumu na  sifa za wajumbe.

Pamoja CHSB, zipo Bodi za Ushauri katika Hospitali za Rufaa za Mikoa (RRHAB).

# Muundo wa Bodi na Kamati

- Bodi na Kamati za Vituo vya Serikali zimeundwa kwa kuzingatia uwakilishi wa makundi na jinsia:
  - Wajumbe wa kuchaguliwa (wanaopiga kura)
    - Watumiaji wa huduma (me na ke)
    - Mwakilishi wa watoa huduma –Huduma binafsi
    - Mwakilishi wa watoa huduma - CSO/FBO/NGO
  - Sekretarieti (Wasiopiga kura)
    - Hili ni kundi la Wataalamu
    - Katibu

# Muundo…

- Miongozo ya uendeshaji wa Bodi na Kamati:
  - Mwongozo wa Bodi za Ushauri za Hospitali, 2016
  - Mwongozo wa CHSB na HFGC, 2013
- Kamati na idadi ya wajumbe
  - Bodi: RRHAB (15) na Halmashauri -CHSB (11)
  - Hospitali:Halmashauri (11), Binafsi (11) na Taasisi/FBO/NGOs (11)
  - Kituo cha Afya: Serikali (9), Taasisi/Asasi za kijamii (8) na Binafsi (8)
  - Zahanati: Serikali (8), Taasisi/Asasi za kijamii (10) na Binafsi (9)

# Majukumu

Bodi na Kamati zitahakikisha:

- Jamii inapata huduma bora, wanazozimudu na zinazoimarisha afya zao
- Upatikanaji na matumizi bora ya rasilimali: fedha,watumishi na vifaa

# Kazi za Bodi na Kamati

- Kujadili mipango ya vituo na taarifa ya utekelezaji wa mipango hiyo (technical and financial)
- Upatikanaji wa rasilimali: watumishi, dawa, vifaa na fedha
  - Kubuni vyanzo vya mapato kwa ajili ya huduma za afya
  - Kuhamasisha jamii kuchangia Mfuko wa Afya ya Jamii
- Kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Afya na kufanya ufuatiliaji.
- Kusaidia kituo katika kupanga na kusimamia masuala ya afya ya jamii
- Kuwasilisha mrejesho kwa jamii

# Hali halisi ya Utendaji wa Bodi na Kamati: Mafanikio na Changamoto

# Vikao wa Bodi (CHSB)

| | Idadi ya Halmashauri | Halmashauri zenye Bodi | Vikao Jan - Machi | Vikao April - Juni | % |
|---|---|---|---|---|---|
| Geita | 6 | 6 | 6 | 6 | 100 |
| DSM | 5 | 5 | 3 | 5 | 100 |
| Lindi | 6 | 6 | 5 | 5 | 83 |
| Mo’go | 9 | 9 | 7 | 8 | 89 |
| Arusha | 7 | 7 | 6 | 6 | 86 |
| Mwanza | 8 | 8 | 8 | 8 | 100 |
| Pwani | 9 | 9 | 9 | 9 | 100 |
| Njombe | 6 | 6 | 5 | 5 | 83 |
| Mbeya | 7 | 7 | 7 | 7 | 100 |
| Kigoma | 8 | 8 | 8 | 8 | |
| Kagera | 8 | 8 | 8 | 8 | 100 |

# Vikao vya Kamati

| MKOA | Idadi ya Vituo | Vituo zenye Kamati | Vikao Jan - Machi | Vikao April - Juni | % |
|---|---|---|---|---|---|
| Geita | 133 | 133 | 133 | 133 | 100 |
| DSM | 117 | 115 | 94 | 110 | 94 |
| Lindi | 242 | 242 | 242 | 242 | 100 |
| Moro | 265 | 265 | 265 | 265 | 100 |
| Arusha | 207 | 207 | 207 | 207 | 100 |
| Mwanza | 279 | 279 | 279 | 279 | 100 |
| Pwani | 328 | 268 | 268 | 268 | 100 |
| Njombe | 225 | 222 | 222 | 222 | 99 |
| Mbeya | 237 | 237 | 237 | 237 | 100 |
| Kigoma | 221 | 221 | 221 | 221 | |
| Kagera | 267 | 267 | 267 | 267 | |

# RRHAB

- Zipo jumla ya Hospitali 28, kati ya hizo 17 zina Bodi
- **Hospitali zenye Bodi**:Mont Meru, Bariadi, Geita, Iringa, Bukoba, Mpanda, Manyara, Musoma, Morogoro, Ligula, Sekou Toure, Sumbawanga, Shinyanga, Kitete, Mawenzi, **Dodoma** na **Mwananyala**
- **Hospitali ambazo hazina RRHAB**: Sokoine, Mbeya, Njombe, Songea, Singida, Songwe, Tumbi, Amana, Maweni, Temeke na Bombo.

# Mafanikio

- Baada ya msukumo wa viashiria vya HBF na RBF Bodi na Kamati zinafanya vikao kila robo.
- Kamati zinashiriki katika usimamizi wa dawa: kupitisha manunuzi na mapokezi ya dawa.
- Kamati zinashiriki katika ukarabati wa vituo unaondelea.
- RRHAB za Tanga na Mbeya zimesaidia kuboresha miundombinu katika Hospitali zao
- Umoja wa bodi za afya Mkoa wa Dar Es Salaam zilifanikiwa kuandaa andiko kwenda benki ya NBC wakapata magari matatu.

# Changamoto

- Kipaumbele katika vikao vinavyofanyika ni kuidhinisha matumizi ya fedha, masuala mengine hayajadiliwi kwa kina.
- Ukaguzi wa miradi haufanyiki kikamilifu
- Wajumbe wanaosimamia ukarabati unaoendelea hawapati posho
- Baadhi ya maeneo hayana wawakilishi wa watoa huduma binafsi pamoja na CSO/FBO/NGO
- Mrejesho kwa makundi yanayowakilishwa hautolewi.

# Changamoto

- Uelewa mdogo wa majukumu: Baadhi ya Bodi zinafanyakazi lakini hazikupata mafunzo na kuzinduliwa rasmi.
- Mkanganyiko wa sheria na miongozo:
  - CHF Act- 2001: 15.-(1) (a ) inaelekeza Bodi kusimamia CHF na lakini kwa maboresho yanayoendelea kazi hii haionekani.
- Baadhi ya Bodi/Kamati kufanya kazi nje ya muda.
- Baadhi ya Vituo binafsi/FBO/NGOs kutokuwa na kamati



- Mchakato mrefu wa kuunda RRHAB

# Nini kifanyike kuimarisha Bodi na Kamati

- Mafunzo kwa Bodi/Kamati:
  - Kila Bodi na Kamati mpya ipewe mafunzo kabla ya kuanza kazi rasmi
  - Kufanyike mafunzo ya mara kwa mara kwa Bodi na Kamati – ikumbukwe kuna wajumbe wapya na makatibu wapya kwenye Bodi na Kamati; wadau wasaidie kugharamia mafunzo haya.
- Yafanyike mapitio ya sheria ya CHF na mwongozo wa CHSB/HFGC ufanyiwe mapitio:
  - Sifa za wajumbe zoboreshwe hasa kigezo cha elimu
  - Usimamizi wa fedha – suala la akaunti ya CHF

# Nini kifanyike kuimarisha Bodi na Kamati

- Halmashauri zipewe maelekezo ya kujumuisha wajumbe wa Bodi wakati wa kukagua miradi ya afya.
- Bodi/Kamati zipewe malengo ya kazi badala ya kupimwa kwa vikao
- Ufanyike uhakiki ili bodi/kamati zilizopitisha zivunjwe kuundwa upya.
- Kamati ziundwe katika vituo binafsi
- RRHAB ipewe mamlaka; isiishie kushauri tu.

# ASANTENI
# KWA
# KUNISIKILIZA